TANGAZO LA SERIKALI Na. 1030 La Tarehe 11/12/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZAWILAYA)

(SURA. 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA HIFADHI YA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli za Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakavyoelekezwa vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji unaozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote;

"maeneo ya malisho" maana yake ni sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri au Kijiji kuwa maeneo ya malisho ya mifugo;

Sura ya 191

"mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ;

"mifugo" maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu;

Sura ya 323

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia kumi na miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia hamsini au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo imetangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli na ni pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hizi.

Masharti kuhusu ufugaji

3.- (1) Mtu yeyote anayefuga katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) kufuga mifugo kwa idadi itakayokuwa imeelekezwa na Halmashauri;

(b) kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;

(c) kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;

(d) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri; na

(f) kuweka alama kwenye mifugo yake kama itakavyolekezwa na Halmashauri.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:
   (a) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
   (b) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;
   (c) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
   (d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri;
   (e) kufuga mifugo kwa zaidi ya idadi iliyoelekezwa na Halmashauri; au
   (f) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata mifugo inayokutwa katika maeneo yasiyoruhusiwa kuchunga, kulisha au kunywesha mifugo.

(4) Halmashauri inaweza, baada ya kupata amri ya Mahakama, kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mifugo hiyo na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo baada ya kutoa gharama za ukamataji, utunzaji wa mifugo .

(5) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kutekeleza mamlaka yake chini kifungu hiki isipokuwa kama hasara hiyo itasababishwa na uzembe wa Halmashauri.

Masharti kuhusu kilimo

4.- (1) Mtu yeyote anayelima katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) taratibu za kilimo kwa kuzingatia kalenda ya kilimo ya Halmashauri na kwa kuzingatia Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi na mazingira;

(b) kutolima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa au maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira;

(c) kutotumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri; na

(d) kutosafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto, isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(2) Kibali cha kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaoruhusiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 4.00 kamili asubuhi na saa 12.00 jioni hadi saa 1.00 usiku.

(4) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo:

(a) kutozingatia kalenda ya kilimo ya Halmashauri;

(b) kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwana au maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira;

(c) kutumia ardhi kinyume na matumizi kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri; au

(d) kusafisha shamba kwa njia ya kuchoma moto bila ya kuwa na kibali au nje ya muda ulioruhusiwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Uchimbaji wa mchanga

**5**.- (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchimba mchanga, kokoto, mawe, udongo au madini yoyote ya ujenzi kwa madhumuni ya kibiashara karibu na makazi ya watu, maeneo ya hifadhi, kandokando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa vyanzo vya maji

6.- (1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa:

(a) kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Halmashauri;

(b) kutoishi katika eneo la hifadhi au chanzo cha maji ndani ya mita sitini;

(c) kutolima, kutokata miti, kutochunga mifugo au kutofanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote eneo lililotangazwa kuwa eneo la hifadhi au chanzo cha maji;

(d) kutoelekeza mabomba ya maji machafu au kujisaidia kupuliza dawa za kuua wadudu kwenye mito, mabwawa, maziwa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji;

(e) kutojimilikisha eneo ambalo ni chanzo cha maji cha umma; au

(f) kutojenga choo cha shimo au jalala la kutupia taka umbali wa chini ya mita sitini kutoka kwenye chanzo cha maji.

(2) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Uhifadhi wa misitu

**7.-** (1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa kuhifadhi na kulinda misitu kwa;

(a) kutokata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka katika Mamlaka husika;

(b) kutochoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika eneo la Halmashauri;

(c) kutovuna miti isipokuwa kwa kibali maalum cha Halmashauri; au

(d) kutovuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum.

(2) Uchomaji wa mkaa utafanyika kwa kibali maalum cha Halmashauri katika maeneo yaliyotengwa mahsusi kwa ajili hiyo.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Utupaji wa taka

8.- (1) Kila mtu katika eneo la Halmashauri atatakiwa kufanya yafuatayo::

(a) kuwa na shimo au chombo maalum cha kuhifadhi taka ngumu na laini; na

(b) kuwa na choo safi na salama;

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Ada ya ukaguzi wa afya

9 (1) Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara.

(2) Viwango vya ada ya ukaguzi wa afya vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwaka wakati wa kuhuisha leseni.

Wajibu wa jumla

10.- (1) Wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira yameharibiwa watakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida eneo hilo kwa kupanda miti na kuendelea kutoharibu mazingira ili kuwezesha uoto au mazingira yarudi katika hali yake ya kawaida kwa kadri watakavyoelekezwa na Halmashauri.

(2) Wakazi wa eneo ambalo moto umetokea katika watakuwa na wajibu wa kushiriki kuzima moto huo kwa kadri watakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Mtu yeyote atakayeshindwa, bila sababu za msingi, kutekeleza maelekezo ya Halmashauri chini ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

11 (1) Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajili ya kutupa taka (dampo) na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji hadi kwenye dampo kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii **(CBOs)** na kuvitambua ili kuviwezesha

kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika makao makuu ya kata na vijiji na maeneo ya mjini baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

(3) Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajiri ya Machinjio ya wanyama.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

12.- Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika eneo, nyumba au jengo lolote kuanzia 12.00 asubuhi hadi 12.30 jioni kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

13.- (1) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hizi atahukumiwa adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa lolote endapo mtu atakiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa kumtoza kiasi kisichozidi shilingi laki mbili baada ya kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu za Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 9(2))*

Ada ya ukaguzi wa Afya

| | AINA YA BIASHARA | ADA KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1 | Baa na maduka ya vinywaji (groceries) | 15,000 |
| 2 | Migahawa, baba na mama lishe | 6000 |
| 3 | Nyumba za kulala wageni (guest house) na hosteli | 15,000 |
| 4 | Kumbi za starehe na mikutano | 20,000 |
| 5 | Maduka | 10,000 |
| 6 | Gereji | 15,000 |
| 7 | Majengo mengine ya biashara | 50,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 1030 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa Chini ya kifungu cha 11(1))*

Ada ya uzoaji takataka

| | ENEO | KIWANGO KWA MWEZI |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za kuishi au makazi kwa kaya | 2000/= |
| 2 | Nyumba za kulala wageni | 5000/= |
| 3 | Maduka | 3000/= |
| 4 | Mgahawa, baba,mama lishe | 2500/= |
| 5 | Hoteli,baa na groceries | 5000/= |
| 6 | Vibanda au meza za biashara | 2000/= |
| 7 | Wachoma chipsi, kuku na nyama | 2500/= |
| 8 | Saluni | 3000/= |
| 9 | Gereji | 5000/= |
| 10 | Fundi seremala, samani | 2500/= |
| 11 | Wauza mbao au karakana za kuranda mbao | 5000/= |
| 12 | Ofisi ya taasisi | 3000/= |
| 13 | Mashine za kusaga na kukoboa | 3000/= |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu chs 13)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi ……………………..…....................……………………………nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ……………………………………... ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Bumbuli kuwa tarehe …..… ya Mwezi …...… Mwaka …........… nilitenda kosa la kukiuka kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Hifadhi ya Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli za mwaka 2020. Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi kiasi cha shilingi na kutimiza wajibu wangu badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu

Leo Tarehe………………… Mwezi…………………Mwaka....................
Jina....................................................................................
Saini......................................................................................

Mbele ya:
Jina: ……………………………………………
Cheo: ………………………………………….
Saini: …………………………………………..

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli uliofanyika mnamo tarehe 19/2/2020 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

GEORGE D. HAULE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bumbuli*

AMIRI A. SHEIZA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Bumbuli*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*